KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

NYUMBA YA ROHO-C. RUTA

Kiitikio

Mungu wangu nikujue mimi, Mungu wangu nikupende
*Mungu nikutumikie, kisha niurithi ufalme Mbinguni * 2*
(wewe) roho umenipa ee, (kisha) ukaihifadhi pazuri
(yaani) ndani ya mwili ee (kwani) mwili ni nyumba ya roho

Mashairi

1. Ndiwe mungu peke yako, wa kuabudiwa ni wewe
   Nishike kitakatifu siku yako (hiyo siku yako)
   nisilitaje kabisa bure jina lako Mwenyezi
   Ulimi wa mwili wangu usiiponze roho yangu

2. Niwaheshimu wazazi, ili nisiwasononeshe
   Uhai wa binadamu niuthamini (yani nisiuue)
   Kuiba nijiepushe, kusema uwongo niache
   Mwili wangu usizini ndipo roho yangu itapona

3. Niepuke kutamani yote yasiyo mali yangu
   Naye mwanamke asiye mke wangu (yani sio wangu)
   Hapo ndipo nitakuwa nimeutumia vizuri
   Mwili ulioiumbia roho ifike Mbinguni juu